# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAISI - TAMISEMI

## SHULE YA SEKONDARI TUKUYU


MKUU WA SHULE: 0753 695 250 PATRON: 0766 758 758

MAKAMU MKUU WA SHULE: 0763 455 191 MATRON: 0754 028 478

SHULE YA SEKONDARI TUKUYU,
S. L. P 27,
TUKUYU.
11/06/2023


**Kumb. Na.TSS/ 0775/JI/ADV/2023/……..**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………...............................................................................**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI TUKUYU HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE MKOA WA MBEYA MWAKA 2023**

1.Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya ……..……

Shule ya Sekondari Tukuyu ipo umbali wa Kilometa 0.5 Kusini mwa Mji wa Tukuyu.Usafiri wa pikipiki kutoka mjini Tukuyu unapatikana katika kituo cha mabasi Tukuyu. Nauli ni Shilingi 1,000/= kwa pikipiki. Aidha unaweza kutembea kwa miguu kutoka stendi hadi Shuleni.

Muhula wa Masomo utaanza tarehe 14/08/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 13/08/2023. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023

**1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**1.1 Sare za Shule**

Sare za shule hii ni nyeusi, golden brown na ugoro kwa Wasichana na Wavulana. Maelezo ya mishono

**1.2 SARE ZA WASICHANA**

✓ Sketi tatu (03)

i. Moja rangi nyeusi na tai yake ndefu
ii. Pili rangi ya golden brown na tai yake ndefu **(Anaweza akashonea shuleni)**

iii. Tatu rangi ya kahawia/ugoro (shamba dress)

**NB:** Unatakiwa uje na sketi tatu zilizoshonwa vizuri na zenye marinda na ndefu zinazokaribia visigino,

**HATUHITAJI SKETI FUPI.**

- ✓ Mashati mawili(2) meupe, yenye mikono mirefu.
- ✓ Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
- ✓ Sare ya Michezo ni bukta moja, track suit nyeusi yenye ufito mweupe, raba jozi moja, kigauni rangi ya blue, soksi ndefu jozi moja rangi ya blue, Tshirt nyekundu isiyo na maandishi, kola, na iwe na mikono mifupi.
- ✓ Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
- ✓ Soksi jozi mbili nyeupe za shule.
- ✓ Masweta mawili (2) rangi ya kijani kibichi yenye shingo umbo la V.
- ✓ Pullneck mbili(2) rangi nyeupe (kuzuia baridi).

## 1. 3 SARE ZA WAVULANA

- ➢ Suruali tatu (3)
  i. Moja rangi nyeusi kitambaa cha tetron na tai yake ndefu.
  ii. Pili rangi ya golden brown na tai yake ndefu (**anaweza akashonea shuleni**)
  iii. Tatu rangi ya kahawia/ugoro **(shamba dress)**

  **NB:** Utatakiwa uje na suruali zote tatu zilizoshonwa vizuri na zenye mifuko mitatu, marinda **(cebrations)** upana miguu ni usiopungua inchi kumi na tano **(15),** hatuhitaji suruali zilizoshonwa mtindo wa jeans. **Ili kuweka kipimo sawa cha sare, mwanafunzi anashauriwa aje na fedha ili ashone akiwa shuleni.**
- ➢ Mashati mawili (2) meupe, yenye mikono mirefu.
- ➢ Sare ya Michezo ni raba jozi moja, bukta moja na track suit nyeusi yenye ufito mweupe isiyo na kofia.
- ➢ Tshirt nyekundu yenye shingo fupi isiyo na maandishi, kola na iwe na mikono mifupi, soksi ndefu jozi moja rangi ya blue.
- ➢ Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
- ➢ Soksi jozi mbili nyeupe za shule.
- ➢ Masweta mawili (2) rangi ya kijani kibichi yenye shingo umbo la V.
- ➢ Pullneck mbili(2) rangi nyeupe (kuzuia baridi).
- ➢ Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

### MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI

- Madaftari makubwa kumi (quire 4) kwa ajili ya masomo yote utakayosoma.
- **Ream (A4)** bunda Mbili (2) kwa mwaka.
- Vitabu vya masomo ya tahasusi husika .
- Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma somo la Biolojia (Biology).
- Scientific Calculator.
- Godoro futi mbili na nusu (2.5) kwa 6.
- Mashuka Jozi 2 ( moja rangi ya bluu bahari na ya pili rangi ya pink)
- Blanket 1 zito, foronya ya godoro 1, chandarua kimoja chenye rangi nyeupe.
- Nguo za ndani za kutosha.
- Vyombo vya chakula (kontena lenye mfuniko), kijiko na kikombe).
- Ndoo 1 ndogo (lita Kumi) na ndoo 1 kubwa (lita 20) zenye mifuniko.
- Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mopa moja na brash ngumu moja

## 2. MICHANGO MBALIMBALI

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha hizo za michango zilipwe kwenye Bank (NMB) Account Namba 61403500086 TUKUYU SECONDARY.** Mwanafunzi anatakiwa alete Pay in Slip Shuleni baada ya kutoa nakala.
**MUHIMU**: **Unatakiwa uje na Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu.**

**3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Kupita njia sahihi uingiapo na utokapo katika eneo la shule kwa ruhusa (Kibali maalumu)

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. Mfano (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xix. Kuruka ukuta au uzio wa shule na kutoka nje ya eneo la Shule bila kibali

**4. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**ZINGATIA: Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**MUHIMU:**

**Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**MKUU WA SHULE: 0753 695 250**
**MAKAMU MKUU WA SHULE: 0763 455 191**
**MWANDAMIZI MALEZI: 0766 758 758**

**"ELIMU NI UKOMBOZI"**
**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI TUKUYU**

**Saini ya Mkuu wa Shule: …………………………………...**

**Jina la Mkuu wa Shule: FARAJI A. MWAKIPUBA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule: ……………………………........**

**Kiambata Na.1**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA:**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:**

**PART A:**

To the medical Officer,
------------------------------------------------
------------------------------------------------
------------------------------ ------------------

From; ----------------------------------------
-------- ----------------------------------------
------------------------------------------------
Date; -----------------------------------------

**Re:** ____________________________________________________________________

Please Examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time Secondary School studies that may also include military training, the Examination should include the following categories **(I-IV)** each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of defect. Pregnant category (**category IV**) will also render a girl candidate ineligible for the cause.

I. (a) Eye sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) General diseases
(e) Leprosy
(f) Epilepsy
(g) Limbs

Other serious disease ---------------------------------------------------------------------------------------
Pregnancy ---------------------------------------------------------------------------------------------------

**PART B: MEDICAL OFFICER:**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have Examined the above named and consider that he/she is physically fit for a full time Secondary school studies.

(a) Eye-sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) General diseases
(e) Leprosy
(f) Epilepsy

II. Neuroses ------------------------------------------------------------------------------------------------

III. Other serious diseases -------------------------------------------------------------------------------

IV. Pregnancy ----------------------------------------------------------------------------------------------

**DATE** ------------------------------------------------ **SIGNATURE** ------------------------------------------------

**STATION** ---------------------------------------------- **DATE** --------------------------------------------------

**Kiambata Na.2**

**OR – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**
**SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:**
**FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI:**

**SEHEMU A:**

1. Jina kamili la mwanafunzi ---------------------------------------------------------------------------

2. Tarehe ya kuzaliwa ----------------------------------------- kabila ---------------------------------

3. Jina la mzazi/mlezi ---------------------------------------------------------------------------------------

4. Uhusiano ------------------------------------------- kazi yake -----------------------------------------

5. Anuani ya Mzazi/Mlezi -----------------------------------------------------------------------------

6. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi ---------------------------------------------------------------------

7. Umbali kuja Shuleni ni KM -----------------------------------------------------------------------
8. Majina ya Ndugu/Walezi wengine wa karibu;-

| JINA | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU | MAHALI ALIPO |
|---|---|---|---|
| (i) | | | |
| (ii) | | | |
| (iii) | | | |
| (iv) | | | |

**TANIBIHI:** Wale wenye picha tu.

9. **MENGINEYO:**
   (Kama mgonjwa aje na uthibitisho wa daktari, kama ni yatima aje na hati ya kifo, kama ni mlemavu, n.k).
   ------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
   ----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

**SEHEMU B:**

**TAMKO LA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:**

Mimi ---------------------------------------------------------------------- (majina matatu) nimezisoma na kuzielewa Sheria, Kanuni na Taratibu za Shule na kwamba niko tayari/ siko tayari kuzifuata.

Sahihi ya mwanafunzi ---------------------------------------- Tarehe --------------------------------------------

**SEHEMU C:**
**TAMKO / AHADI YA MZAZI/ MLEZI:**

Mimi --------------------------------------------------------------- ambaye ni Mzazi / Mlezi wa mwanafunzi ----------------------------------------------------------- ninaahidi kwamba nitatekeleza / sitatekeleza maagizo na mahitaji yote muhimu ya Shule kama nilivyoelekezwa na kwamba niko tayari / siko tayari kushirikiana na Uongozi wa Shule katika suala zima la malezi na maadili mema ya mtoto wangu ili kuinua taaluma na nidhamu yake. Pia ninakubali kutii Taratibu, Kanuni na sheria zote za shule na kulipa Ada na michango mingine kama ilivyoelezwa pia ntafuata maelekezo mengine kadri yatakavyotolewa na uongozi wa Shule ya Sekondari Tukuyu.

Sahihi ya Mzazi / Mlezi ------------------------------------------------- Tarehe --------------------------------

**Kiambata na. 3**

**OR - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE:**
**SHULE YA SEKONDARI TUKUYU:**

## TAMKO LA UTII WA SHERIA ZA SHULE:

## KIAPO CHA MWANAFUNZI:

Kuwa mimi ……………………………………………………………. Nikiwa ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Tukuyu, nimekubali kuishi katika jumuiya hii nikiwa mtiifu na kufuata sheria zote za shule kwa mujibu wa **sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978** kama ilivyorekebishwa na **sheria Na. 10 ya mwaka 1995.** Bodi ya shule imepewa mamlaka ya kusimamia nidhamu ya wanafunzi. Hivyo, ninaahidi kufuata utaratibu wote ulioainishwa kwenye sheria za shule wakati wote ninapokuwa mwanafunzi wa shule hii.

Hivyo nikiwa ni mwanafunzi wa kidato cha ------------------------------ Tahasusi ya………… katika Shule ya Sekondari Tukuyu ninaapa kutomiliki Simu ama kifaa chochote kinachoashiria kumiliki **Simu** pamoja na urukaji **uzio/ukuta** (fence) wa shule pia kutoshiriki mgomo , fujo au kuanzisha mgomo au fujo. Ninaahidi kuwa mtiifu na mwanafunzi mwenye adabu kwa walimu wangu wote na watumishi pamoja na wanafunzi wenzangu wa jumuiya ya Shule Sekondari Tukuyu ili niweze kufaulu masomo yangu vizuri.

Pia leo tarehe ----------- mwezi-------------------- mwaka--------------------- ninaahidi kuwa nikikamatwa na **Simu** ama kifaa chochote kinachoashiria mimi kumiliki simu na nimeruka **uzio/ukuta** (fence) wa shule pamoja na makosa mengine ambayo ni kinyume na Taratibu, Kanuni na Sheria za shule nifukuzwe shule kabisa.

Mimi ------------------------------------------------------------------------------ (majina matatu).

Sahihi ------------------------------------------ leo tarehe -------------------------------------------

Mbele ya mkuu wa Shule ya Sekondari Tukuyu kwa niaba ya Bodi ya Shule ya Sekondari Tukuyu.

**---------------------------------------------**
**MWAKIPUBA, F. A**
**(MKUU WA SHULE)**

**Kiambata na. 4**

**OR – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**
**SHULE YA SEKONDARI TUKUYU**
**TAARIFA ZA NDUGU (WAZAZI/WALEZI) WA MWANAFUNZI WATAKAORUHUSIWA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI.**

| | |
|---|---|
| **1.** JINA: ………………………………….. | 2. JINA: ………………………………………………… |
| JINSI: …………………………………… | JINSI: ………………………………………………… |
| UHUSIANO: ………………………………… | UHUSIANO: ……..………………………………… |
| ANAKOTOKA: ………………………… … | ANAKOTOKA: …………………………………….. |
| ANUANI: ………………………………….. | ANUANI: …………………………………………… |
| NA. YA SIMU: ……………………………… | NA. YA SIMU: ……………………………………… |
| Picha | Picha |

| | |
|---|---|
| **3.** JINA: ………………………………….. | 4. JINA: ………………………………………………… |
| JINSI: ……………………………. | JINSI: ………………………………………………… |
| UHUSIANO: …………………………. | UHUSIANO: ………………………………………… |
| ANAKOTOKA: ……………………… | ANAKOTOKA: …………………………………….. |
| ANUANI: ……………………………. | ANUANI: …………………………………………… |
| NA. YA SIMU: ……………………… | NA. YA SIMU: ……………………………………… |
| Picha | Picha |

Mimi ………………………………………………………………….. (Mwanafunzi) kidato cha ……………… kuanzia mwaka wa masomo …………….. hadi …………… Nathibitisha kuwa watajwa na wenye picha hapo juu ni Wazazi/Walaezi/Ndugu zangu watakaonitembelea muda wote nitakapokuwa katika shule hii ya Tukuyu Sekondari.

**Sahihi …………………………** **Tarehe …………………………..**